

CHUO CHA AFYA KARATU

Barua pepe:

karatuhealthtraining2012@gmail.com

info@karatuhti.ac.tz

Tovuti: www.karatuhti.ac.tz



S.L.P.165

KARATU- ARUSHA

USAJILI WA NACTE

NI:

REG/HAS/113

WITO WA KUJIUNGA NA CHUO CHA AFYA KARATU (KARATU HEALTH TRAINING INSTITUTE) MWAKA WA MASOMO 2026/2027

NDG:.....

Salamu.

Tunapenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Chuo cha Afya Karatu (Karatu Health Training Institute) katika fani ya **UTABIBU/UUGUZI**. Siku ya kuripoti ni kuanzia tarehe **14/10/2026** hadi **29/10/2026** kuanzia 3:00 Asubuhi hadi saa 10:00 jioni. Masomo na wiki ya ufahamu wa mazingira (orientation week) yataanza tarehe **21/10/2026 hadi 29/10/2026**

Kwa mawasiliano tumia anwani ya barua pepe hapo juu na Namba za simu kama zinavyoonekana hapa chini.

No. +255 737 768 644, 0754 824 854 ,0768 861 915 na 0752 743 541

1. **MUDA WA MAFUNZO:** Mafunzo ni Miaka mitatu (3)

2. **WAKATI UTAKAPOKUJA CHUONI UFIKE NA VITU VIFUATAVYO BILA KUKOSA:**

(A) Ada. (MWANAFUNZI HATAPOKELEWA BILA KUJA NA STAKABADHI YA MALIPO)

(B) Cheti halisi cha Elimu ya Sekondari (Form Four) na Cheti cha Kuzaliwa (Birth Certificate).

(C) Shuka za kulalia jozi 2, blanketi 1, Godoro nchi 2 ft 6, Foronya 2, mto 1, Taulo 1 au 2 na bedcover 2- rangi ya pinki (Wasichana) na bluu (Wavulana), chandarua 1, ndoo 1,

(D) Biblia au Misale ya waumini au Quaran kulingana na imani yako.

(E) Picha "Passport size" 2 uliyopiga hivi karibuni yenye rangi ya bluu kwa nyuma (Blue background) pamoja na picha ya Mzazi/Mlezi anayekulipia Ada. (Passport size) 2

(F) Kalamu, penseli, rula na mifuto, Counter book 8, daftari ndogo 5, futi kamba ya kupimia nguo (tape measure), Kipima Joto (Clinical Thermometer yenye zebaki na siyo digital), BP Machine (manual na siyo digital) pamoja na Stethoscope, Pen torch na patella hammer

(G) Saa ya mkononi yenye mshale wa sekunde

(H) Vyombo vya kulia chakula. Sahani 1, bakuli 1, kijiko 1 na kikombe cha chai 1

(I) Compyuta mpakato (Laptop) ni kifaa muhimu katika masomo kama uwezo wa mzazi utaruhusu.

3. SARE ZA WANAFUNZI

Sare za Chuo zinapatikana chuoni, hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni na kiasi cha Tshs. 170,000/ kwa ajili ya sare. Mwanafunzi atapewa jozi (pair) mbili za sare za chuo ambazo ni kama ifuatavyo:

UUGUZI NA UKUNGA

Wasichana: T-shirt moja ya Chuo, Gauni jozi 2 na sweta jozi 2, isipokuwa aje na Viatu vyeusi vyenye gidamu jozi 2 na soksi nyeupe jozi 2, "viatu visiwe vyenye kupiga kelele utembeapo".

Wavulana: T-shirt moja ya Chuo, Kaunda suti jozi 2, suruali jozi 2, na sweta jozi 2, isipokuwa aje na viatu vyeusi jozi 2 na soksi nyeupe jozi 2.

UTABIBU: Mwanafunzi aje na viatu vyeusi jozi 2 na soksi nyeupe jozi 2, sare zingine atapewa chuoni ambazo ni kama ifuatavyo:

Wavulana: Suruali jozi 2, sweta jozi 2, shati jozi 2, clinical coat na Tshirt moja ya chuo

Wasichana: Gauni jozi 2, sweta 2, clinical coat na Tshirt moja ya chuo

○ **Tahadhari:** - *Jeans haziruhusiwi kuvaliwa darasani au wakati wa mazoezi kwa vitendo Hospitalini*

- *Nguo yeyote ya kubana haitakiwi kabisa chuoni.*
- *Unasisitizwa kuja na vifaa vyote unavyopaswa kuja navyo.*

NB:

- Uje na fomu hii pamoja na namba utakayotumiwa na **NACTVET** siku ya kuripoti chuoni

SHERIA ZA CHUO.

Sheria za Chuo zilizoordheshwa hapa chini ni lazima zifuatwe na wanachuo wote waliokubaliwa kujiunga na Chuo hiki. Mwanafunzi atakayevunja mojawapo ya sheria hizi atakuwa amefanya kosa kubwa ambalo linaweza kusababisha kusitishiwa na pengine kuachishwa masomo.

Wazazi wa mwanafunzi wanaombwa kuzisoma sheria za Chuo na kuzielewa kabla ya kumruhusu mtoto kujiunga na Chuo hiki. Nia na makusudi ya sheria hizi ni kutaka kuweka Chuo, Hospitali na kazi yenyewe ya Uguzi/Utabibu katika hali ya sifa njema daima.

SHERIA:

- i. Wanafunzi wanaruhusiwa kutembelea Hospitali wakati wanapopumzika katika saa ambazo zimewekwa kuwaona wagonjwa. Ni lazima mwanafunzi anapokuwa Hospitalini (Clinical area) awe na sare ya Chuo.
- ii. Wanafunzi wakiruhusiwa kwenda nje ya maeneo ya chuo wanatakiwa kurudi Chuoni kabla ya saa 12:00 jioni.
- iii. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea nyumba za wafanyakazi.

- iv. Wageni hawaruhusiwi kwenda kuwatembelea wanafunzi katika maeneo ya bweni na katika maeneo ya darasani na wodini
- v. Mgeni anayetaka kuonana na mwanafunzi ni sharti afike ofisini kwa utambulisho na hivyo kupewa kibali cha kuongea na mwanafunzi katika eneo lililotengwa.
- vi. Mwanafunzi **ni lazima** alale peke yake katika kitanda alichopewa.
- vii. Mwanafunzi wanaokaa chuoni hawaruhusiwi kurudi nyumbani mpaka wakati wa likizo, kama kutakuwa na umuhimu wa mwanao kuja nyumbani, taarifa zote zisizo za kawaida lazima zipitie kwa **Mkuu wa Chuo au mtu yeyote aliyeidhinishwa na chuo. Tafadhali usiwasiliane na mwanafunzi moja kwa moja.**
- viii. Ruhusa itatolewa tu endapo mwanafunzi amefiwa na wafuatao; Baba mzazi, Mama mzazi na ndugu wa kuzaliwa na Mlezi.
- ix. Kila mwanafunzi anatakiwa awe na tabia njema popote atakapokuwa kukiletea sifa njema Chuo, Hospitali, fani za Afya na jamii kwa ujumla.
- x. Likizo itatolewa mara moja kwa Mwaka kulingana na ratiba ya Wizara ya Afya na baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET). Mwanafunzi anatakiwa kuripoti katika muda unaotakiwa, ama sivyo sheria za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake. Wanafunzi watakuwa na mapumziko mafupi mwisho wa muhula wa kwanza. Endapo mwanafunzi atabaki Chuoni wakati wa likizo inabidi achange gharama za malazi na Chakula
- xi. Yafuatayo ni baadhi ya mambo yasiyokubalika Chuoni: -
 - a. **Ulegevu:** Katika kazi na masomo, ukaidi, kukosa nidhamu na kutoshirikiana na wengine masomoni na kazini.
 - b. **Kupayukapayuka - Chuoni, Bwenini au Hospitalini.**
 - c. **Ulevi:-** Pombe ni mwiko kuonekana bwenini, Chuoni au Hospitali.
 - d. **Wizi** wa aina yoyote haukubaliki.
 - e. **Kujitibu mwenyewe** ni mwiko kwa mwanafunzi yeyote.
- xii. Mwanafunzi wa kike haruhusiwi kuingia katika bweni la mwanafunzi wa kiume kadhalika mwanafunzi wa kiume haruhusiwi kuingia katika bweni la wanafunzi wa kike.
- xiii. Kila mwanafunzi atalazimika kufanya usafi wa Bweni na Chuo. Na wakati wote vitanda viwe vimetandikwa vizuri.
- xiv. Hakuna ruhusa kwa mwanafunzi yeyote kuingiza chakula cha aina yeyote katika bweni.
- xv. Kila mwanafunzi awe na mfuko wa kuweka nguo chafu kabla ya kuzifua. Vitu visiwe sakafuni ili kurahisisha usafi wa bweni kufanyika sawasawa.
- xvi. Mwanafunzi anapaswa kutunza na kutumia kwa uangalifu mkubwa vifaa vyote anapokuwa Hospitali na mahali popote Chuoni. Kuta zisipigwe misumari au kuweka picha yeyote ndani ya bweni au darasani. Anapaswa kutoa taarifa mara moja anapoharibu kitu chochote au akiona kitu chochote kilichoharibika ili matengenezo yaweze kufanyika mapema au kitu kingine kiwekwe badala yake.
- xvii. Taa zizimwe saa 4.00 usiku, milango ya madarasa ifungwe na mtu wa mwisho kujisomea usiku kuepuka kutofautiana na Walinzi wa usiku. ukibainika kwenda kinyume adhabu kali itatolewa dhidi yako.

- xviii. Kila mwanafunzi ana wajibu wa kufua nguo zake mwenyewe na usafi wake kwa ujumla. Nguo zitapigwa pasi eneo lililotengwa ndani ya bweni na siyo ndani ya vyumba vya kulala.
- xix. Chuo hakitagharamia matibabu ya mwanafunzi hivyo wenye kadi za Bima ya Afya wafike nazo Chuoni kwa ajili ya matibabu. Wasio na Bima ya Afya ni **LAZIMA** waje na fedha shilingi 50,400/- kama ilivyoinishwa katika jedwali hapo chini kwa ajili ya bima ya afya. Fedha hii haitaingia kwenye mfuko wa Chuo.
- xx. Endapo kwa bahati mbaya mwanafunzi atafariki akiwa Chuoni gharama za kusafirisha mwili zitapangwa na chuo kwa kushirikiana na mzazi au mlezi.
- xxi. Ili kutambua mzazi/mlezi wa Mwanafunzi Chuo kinaagiza kila mwanafunzi aje na picha ya wazazi/walezi.
- xxii. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na simu ya mkononi darasani au wadini.
- xxiii. Kila mwanafunzi ashiriki kikamilifu katika Elimu ya kujitegemea na pia katika vikundi vya utamaduni na michezo ambavyo amevichagua mwenyewe, hii ni sehemu mojawapo muhimu katika masomo.
- xxiv. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na bidii katika masomo, kila somo afaulu kuanzia 60% na kuendelea . **Hatukubaliani na mwanafunzi mvivu kitaaluma.**
- xxv. Kila mwanafunzi atakaye feli somo/masomo atalipia **Tshs. 200,000/=** ikiwa ni gharama za kurudia mtihani kama mtihani unafanyika chuoni aidha gharama hizi zinaweza kuongezeka kulingana na mahali iwapo mitihani itafanyika nje ya chuo kulingana na miongozo au maelekezo ya wizara ya Afya.
- xxvi. Mwanafunzi akiwa maeneo ya kufanyia mazoezi kwa vitendo ni lazima aage kwa mkuu idara/kitengo husika kabla hajaondoka. Mwanafunzi haruhusiwi kuonana na mgeni wake awapo idarani au darasani.
- xxvii. Rangi za kucha, rangi za midomo, rangi za nywele, curl, relaxer na rasta haziruhusiwi kabisa

4.ADA

A. MCHANGANUO WA ADA NI KAMA IFUATAVYO: -				
NA.	KIPENGELE	MWAKA WA KWANZA	MWAKA WA PILI	MWAKA WA TATU
1.	ADA	1,160,000.00	1,160,000.00	1,160,000.00
2.	FEDHA ZA TAHADHARI (Fedha hizi hazirudishwi)	60,000.00	60,000.00	60,000.00
3.	MITIHANI YA NDANI	300,000.00	300,000.00	300,000.00
4.	VIFAA/GHARAMA WAKATI WA MAFUNZO KWA VITENDO	250,000.00	250,000.00	250,000.00
	JUMLA KUU	1,770,000.00	1,770,000.00	1,770,000.00

B. MALIPO MENGINEYO				
NA.	KIPENGELE	MWAKA WA KWANZA	MWAKA WA PILI	MWAKA WA TATU
1.	VITABU VYA MAZOEZI	80,000.00	80,000.00	80,000.00
2.	UTAFITI	-	-	100,000.00
3.	KITAMBULISHO	10,000.00	-	-
6.	SERIKALI YA WANACHUO	20,000.00	20,000.00	20,000.00
	JUMLA KUU	110,000.00	100,000.00	200,000.00

FEDHA hizi zilipwe katika Akaunti ifuatayo:

Jina la Akaunti ya Chuo: **ELCT-ND. KARATU HEALTH TRAINING INSTITUTE**

Namba ya akaunti: **40910006084.**

NMB Tawi la Karatu au

ELCT-ND. KARATU HEALTH TRAINING INSTITUTE

Namba ya akaunti: **00220100012**

Uchumi Commercial Bank (UCB)

Tawi la Karatu

C. CHAKULA (kwa wanafunzi Chuoni).				
NA.	KIPENGELE	MWAKA WA KWANZA	MWAKA WA PILI	MWAKA WA TATU
1.	CHAKULA	800,000.00	800,000.00	800,000.00

Fedha za chakula zilipwe kupitia akaunt hii.

Jina la Akaunti: **ELCT-ND. KARATU HEALTH TRAINING INSTITUTE**

Namba ya akaunti **40906600065**

NMB

Tawi la Karatu

****Muhimu****

- Fedha kwa ajili ya ada na malipo mengine ziwekwe kwenye account ya Chuo
- Kwa mwaka wa tatu kila mwanafunzi atachangia kiasi cha TZS 200,000 kwa ajili ya mahafali
- Kwa Mwanafunzi aliyelipia chakula, atakapokwenda mazoezi kwa vitendo nje ya Chuo atapewa chakula na usafiri na atajigharamikia malazi yake.

D. FEDHA ZINAZOLIPWA KWENYE MAMLAKA ZA USIMAMIZI.

NA.	KIPENGELE	MWAKA WA KWANZA	MWAKA WA PILI	MWAKA WA TATU
1.	NACTVET	20,000.00	20,000.00	20,000.00
2.	BIMA YA AFYA	50,400.00	50,400.00	50,400.00
3.	MTIHANI WA WIZARA	150,000.00	150,000.00	150,000.00
	JUMLA KUU	220,400.00	220,400.00	220,400.00

Fedha hizi zilipwe kwa awamu mbili, ambapo fedha ya NACTVET na BIMA italipwa wakati wa kuripoti chuoni na fedha ya mitihani ya wizara italipwa wakati wa kufanya malipo ya awamu ya mwisho ya chuo (mwezi wa sita) na zitalipwa kwa kupitia akaunti hii.

Jina la Akaunti: **ELCT-ND. KARATU HEALTH TRAINING INSTITUTE**

Namba ya akaunti 40906600065

TAWI LA NMB

6. MALAZI/BWENI

- Huduma ya hostel itakuwa ni bure kwa wanafunzi watakaowahi kuripoti Chuoni. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kulala nje ya Chuo, isipokuwa pale endapo mabweni yatakuwa yamejaa.
- Mwanafunzi atakayeishi katika bweni za chuo atahitajika kusaini mkataba wa makubaliano kabla ya kupewa chumba.
- Kila chumba kitakuwa na kitanda tu hivyo mwanafunzi atalazimika kuja na godoro lake, blanketi, mashuka na net kwa ajili ya kujikinga na mbu.
- Mwanafunzi haruhusiwi kupika chakula cha aina yoyote ndani ya bweni la chuo.

7. MWONGOZO WA ULIPAJI WA ADA YA CHUO NA GHARAMA NYINGINE KWA AWAMU

MALIPO AWAMU YA KWANZA (SIKU YA KURIPOTI CHUONI)

	MWAKA WA KWANZA	MWAKA WA PILI	MWAKA WA TATU
ADA TU	597,500	587,500	687,500
ADA NA CHAKULA	872,500	862,500	962,500

MALIPO AWAMU YA PILI (MWEZI JANUARY)

	MWAKA WA KWANZA	MWAKA WA PILI	MWAKA WA TATU
ADA TU	427,500	427,500	427,500
ADA NA CHAKULA	702,500	702,500	702,500

MALIPO AWAMU YA TATU (MWEZI APRIL)

	MWAKA WA KWANZA	MWAKA WA PILI	MWAKA WA TATU
ADA TU	427,500	427,500	427,500
ADA NA CHAKULA	702,500	702,500	702,500

MALIPO AWAMU YA NNE (MWEZI JUNI)

	MWAKA WA KWANZA	MWAKA WA PILI	MWAKA WA TATU
ADA TU	427,500	427,500	427,500
ADA NA CHAKULA	702,500	702,500	702,500

- i. Siku ya kuja kuanza masomo mwanachuo anatakiwa kuja na stakabadhi ya malipo (BANK PAY IN SLIP) ndipo atakapopokelewa chuoni
- ii. Kila Mwanafunzi atakuja na Rim paper (A4) moja aina ya (paper premiumMulti – purpose paper) kwa kila mhula.Kwa wale ambao watashindwa kufika na aina hiyo Rim paper zinapatikana chuoni kwa Tsh 15,000 .
- iii. Ada ya Mitihani ya Wizara pamoja na NACTVET na Bima ya Afya (NHIF) italipwa kwenye akaunti ya chuo na chuo kitalipa mamlaka husika baada ya kupata control namba kutoka mamlaka husika, **Kiasi cha Tshs. 220,400/=kama ilivyoainishwa katika jedwali “D” hapo juu.**
- iv. Ni jukumu la Mzazi/Mlezi kutoa Ada na siyo mwanafunzi kufuatilia Ada na kuacha masomo.
- v. Ada ikishalipwa hairudishwi.
- vi. Malipo yatakayo zidi yatarudishwa mwisho wa mafunzo kwa mwanafunzi kuomba kwa barua
- vii. **Tunaomba Mzazi uzingatie ulipaji wa ada ili kuondoa usumbufu wa kumrudisha nyumbani Mwanafunzi.** Hii itamuathiri kisaikolojia na pia kuingilia ratiba na masomo yake. Kumbuka siku ishirini na moja kwa mwaka nje ya masomo itampasa kuachishwa Chuo.

(Chuo kinakuomba ushirikiano wako katika hili.)

8. UTARATIBU WA MAFUNZO:

- i. Mafunzo ni kwa nadharia na vitendo- kila mwisho wa muhula kutakuwa na mtihani wa nadharia na vitendo ambapo mwanafunzi atatakiwa afaulu zaidi ya asilimia 50 kwa kila somo. Pungufu ya hapa atatakiwa kulipia kurudia mtihani huo **Tshs. 200,000** na akishindwa atalazimika kurudia muhula mzima, akishindwa tena atarudia mafunzo kulingana na miongozo ya wizara ya Afya na NACTVET.
- ii. Mwanafunzi atakayeshindwa mtihani wa mwisho wa muhula chini ya wastani wa ufaulu wa GPA 2.0 ataachishwa masomo.
- iii. **Mwanafunzi afikapo mwaka wa pili, atapaswa kufanya mafunzo yake ya vitendo nje ya Chuo kwa muda usiozidi wiki tatu. Mzazi atapaswa kulipia gharama kulingana na wakati na mahali kama itakavyojulikana kwa gharama za wakati huo.**
- iv. Endapo mwanafunzi hatahudhuria masomo siku 14 mfululizo kwa muhula anakosa vigezo vya kuendelea na masomo kulingana na sheria za wizara na NACTVET na Chuo.
- v. Endapo mwanafunzi hatahudhuria masomo siku 14 kwa sababu ya ugonjwa atarudia muhula.
- vi. Mwanafunzi yeyote anapovunja sheria za Chuo na Wizara ya Afya na baraza la Taifa la Elimu na mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) atachukuliwa hatua za kinidhamu, ikiwa ni pamoja na kuachishwa masomo kulingana na ukubwa wa kosa.
- vii. Mwanafunzi anaporudia muhula kwa sababu yakushindwa masomo au utovu wa nidhamu atalipa ada upya. Anapoachishwa masomo **“ADA HAITARUDISHWA”**
- viii. Mwanafunzi ambaye amefeli muhula, na akiwa anaendelea na masomo wakati anasubiri mtihani wa marudio ni lazima kulipa ada ya muhula husika wa masomo na endapo matokeo yake ya mtihani wa marudio hayatakuwa mazuri **“ADA HAITARUDISHWA”** na atalipa ada upya wakati wa kurudia muhula aliofeli.
- ix. Endapo mwanafunzi atafeli mtihani wa mwisho wa muhula wa pili na atakikiwa kurudia mtihani huo nje ya chou atajigharamia mwenyewe gharama za malazi na chakula kwa kipindi chote atakapokuwa anafanya mitihani hiyo.
- x. Ni lazima kila mwanafunzi awe na BIMA ya afya, Hivyo mzazi atalazimika kulipia bima ya afya wakati wa kuripoti endapo mtoto hana BIMA ya afya.

NB: Ni muhimu mwanafunzi azingatie sheria za Chuo na kufanya bidii katika masomo.

9. MAKUBALIANO YA MWANAFUNZI PAMOJA NA MZAZI/MLEZI

Mzazi/Mlezi wako aisome na kuweka sahihi yake sehemu ya chini baada ya mwanafunzi kusoma, kukubali na kujaza sehemu husika.

Mimi:(Jina la Mwanafunzi)

-
- i. Ninakubali/sikubali kuchukua mafunzo ya utabibu kwa kipindi cha kuanzia.....mpaka.....
 - ii. Naahidi kutii sheria za chuo na Hospitali.
 - iii. Nitakuwa tayari kula chakula ambacho kitapatikana chuoni
 - iv. Ninaahidi kushiriki kikamilifu katika Elimu ya kujitegemea
 - v. Nitafanya bidii katika masomo na kazi, nitakuwa na nidhamu, Nitawaheshimu wakuu wangu wa Chuo na Hospitali na Wakuu wengine wote
 - vi. Nitajiunga na kikundi cha Netball/Mpira wa Miguu/Wavu/utamaduni na Uimbaji ili kuimarisha Afya. Weka alama ya $\sqrt{\text{(vema)}}$ panapostahili

Uthibitisho:

Sahihi ya Mwanafunzi.....

Jina la Mzazi/Mlezi.....

Sahihi ya Mzazi/Mlezi.....

Tarehe ya Kuweka sahihi.....

NB: Soma vizuri sheria za Chuo kabla ya kuweka sahihi katika fomu hii.

Fika na fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu unaporipoti chuoni

.....


Dkt. LIASI SIRIAGI
MKUU WA CHUO

